BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Nne – Tarehe 09 Mei, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Ikulu:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - Ikulu kwa mwaka 2026/2027.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - Ikulu kwa Mwaka 2026/2027.

## II. MASWALI:

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

419. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Vitengo vya Manunuzi vipo chini ya Wizara ya Fedha;

Ni lini Serikali itafanya mabadiliko ya mizunguko (Rotation) kwa Wafanyakazi wa Kitengo cha Ununuzi, kama ilivyo kwa Wahasibu na Wakaguzi.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

438. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Ubadilishaji wa mita zinazoharibika ni utaratibu unaotumika katika Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO).

Je, kuna hatua zipi zinazochukuliwa wakati wa ubadilishaji wa mita hizo.

**Wizara ya Kazi na Uwekezaji:**

295. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Kwa kuwa kila Wizara huhitaji kujitegemea ili kuepuka mgongano au muingiliano wa majukumu na Wizara nyengine. Na kwa kuwa, kwa mitazamo ya baadhi ya wananchi wanaona kuwa, kuna wakati Wizara moja inaingiliana kimajukumu na Wizara nyengine kuhusiana na suala zima la kazi na ajira,

Je, kuna tofauti gani ya utekelezaji wake baina ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji na Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji.

**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:**

200. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Kwa kuwa Sekta ya Mawasiliano ni sekta muhimu sana katika zama hizi za sayansi na teknolojia. Na kwa kuwa sekta hii ni ya Muungano na ni miongoni mwa inayolalamikiwa kuikosesha Zanzibar fursa nyingi ambazo zingepelekea kuisaidia Serikali na wananchi wake kukuza uchumi wao.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani ya kukaa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kujadili juu ya suala la upatikanaji wa kimitandao ndani ya Zanzibar.

(b) Kwa kuwa TCRA huichukulia Zanzibar kama eneo tu la mawasiliano na si nchi iliyoungana, kwa nini Serikali haiiondoi Sekta ya Mawasiliano katika mambo ya Muungano kutokana na Zanzibar kukosa haki zake moja kwa moja.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

393. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

(a) Mbali na nyongeza ya mshahara inayotolewa na Rais, ni kitu gani cha msingi kilichofanyika kwa upande wa maslahi ya walimu, tokea Mheshimiwa Waziri ulipoteuliwa kushika madaraka ya kuiongoza Wizara hii.

(b) Mbali na nyongeza ya nauli za walimu, je, Serikali imejipanga vipi kuongeza posho na kwa kiwango gani.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

283. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Kwa kuwa kuna miradi mingi inayotekelezwa na wawekezaji na kusimamiwa na Serikali hapa Zanzibar;

Je, kwa kiasi gani miradi hiyo inazalisha ajira za muda mfupi kwa vijana wazalendo wa Zanzibar, hususani kazi ambazo hazihitaji utaalamu wala ujuzi maalumu.

**Wizara ya Afya:**

237. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi): Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na ongezeko kubwa la watoto wanaozaliwa na kugundulika kuwa na Usonji (Austim) hapa Zanzibar, ambapo licha ya ukubwa wa tatizo hilo, Wizara ya Afya imekuwa ikiwapa matibabu watoto hawa katika hospitali ya wagonjwa wa akili iliyopo Kidongo Chekundu, na kukosa vituo sahihi ambavyo vinahusika na matibabu na kliniki za ugonjwa huu.

(a) Je, ni ipi takwimu sahihi ya watoto wenye ugonjwa wa Usonji hapa Zanzibar.

(b) Je, Wizara yako ina wataalamu wangapi wa *Neuro-Developmental Pediatrician* pamoja na *Speech Therapist* na katika vituo gani.

(c) Je, ni zipi sera na progamu maalum za kitaifa za Serikali katika kukabiliana na ugonjwa huu.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

25. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Pamoja na kuimarika kwa uvuvi hapa nchini bado kumekuwepo na kiwango kikubwa cha kuingiza samaki kutoka nje ya nchi ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani. Hali hii inathibitisha kuwepo kwa pengo kati ya mahitaji ya samaki na kiwango cha uzalishaji wa ndani.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wavuvi wa Zanzibar wanavua kwa kiwango cha kutosha ili kukidhi mahitaji ya ndani.

(b) Je, Serikali ina mkakati gani mahususi wa kuhakikisha Sekta ya Uvuvi inachangia ipasavyo katika kupatikana ajira kwa vijana na wanawake.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

256. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

(a) Je, Serikali inakusanya mapato ya kiasi gani kupitia Kivutio cha Utalii cha Kisiwa cha *Prison* ambacho kina urithi wa kihistoria.

(b) Ni utaratibu gani unaotumika katika ukusanyaji na ugawaji wa mapato ya kisiwa hicho kati ya mwekezaji na Serikali.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Ikulu:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - Ikulu kwa mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**09 Mei, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**WAWAKILISHI, ZANZIBAR**